Mwananchi, Ijumaa Machi 15, 2024.

# AG apewa miezi 12 kurekebisha sheria ya ukomo

Daniel Mjema, Mwananchi
dmjema@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Mahakama Kuu imeiamuru Serikali kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), kukifanyia marekebisho kifungu cha 44 (1) na (2) cha Sheria ya Ukomo wa Kufungua Mashauri (LLA) kwa kuwa kinakiuka Katiba ya Tanzania.

Jopo la majaji watatu waliosikiliza shauri namba 12 la 2023 lililofunguliwa na Joram Bashange dhidi ya AG pamoja na Waziri wa Katiba na Sheria, wamesema vifungu hivyo vinakiuka haki ya msingi ya usawa mbele ya sheria, haki ya kusikilizwa na haki ya kukata rufaa.

Kifungu hicho cha LLA cha sheria hiyo ya ukomo sura ya 89 ya mwaka 1971 kama kilivyofanyiwa marejeo na Bunge mwaka 2019, kinampa waziri mwenye dhamana ya Katiba na Sheria, mamlaka kuongeza muda wa kufungua shauri mahakamani.

Kulingana na kifungu hicho, ikiwa waziri ana maoni kwa kuzingatia mazingira ya kesi, anaweza baada ya kushauriana na AG, kutoa amri ya kuongeza muda wa ukomo wa kufungua shauri na muda huo utahesabika ndio ukomo wa shauri hilo.

Katika hukumu yao waliyoitoa Machi 13, 2024, majaji hao, Dk Yose Mlyambina, Edwin Kakolaki na Dk Ubena Agatho, wameipa Serikali muda wa miezi 12 kukifanyia marekebisho kifungu hicho kwa lengo la kuondoa upungufu uliobainika.

Kulingana na uamuzi wa majaji hao wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Masjala kuu ya Dar es Salaam, endapo Serikali itashindwa kukifanyia marekebisho kifungu hicho ndani ya muda huo wa miezi 12, kifungu hicho kitaondolewa kwenye vitabu vya sheria.

Majaji katika hukumu yao wamesema vifungu hivyo 44(1) na (2) vya sheria hiyo ni batili kwa kuwa vinakiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 na marekebisho yake, kutokana na kutoa uwezekano wa kutoa upendeleo.

Vilevile, majaji hao wamesema vifungu hivyo pia havitoi haki ya msingi ya kusikilizwa na kinaukandamiza upande wa pili wa shauri husika, kwa kuwa haushirikishwi katika amri hiyo ya waziri ya kuongeza muda, hivyo kutokuwepo usawa katika sheria.

"Masharti haya yanaleta hali ya mzaha katika kulinda taratibu dhidi ya matumizi mabaya ya mamlaka aliyopewa mdaiwa wa kwanza (waziri). Hivyo, kukosa mchakato na zaidi ya yote hakuna haki ya kukata rufaa inayotolewa," wamesema majaji hao.

> **"Masharti haya yanaleta hali ya mzaha katika kulinda taratibu dhidi ya matumizi mabaya ya mamlaka aliyopewa mdaiwa wa kwanza (waziri). Hivyo, kukosa mchakato na zaidi ya yote hakuna haki ya kukata rufaa inayotolewa."**
>
> Hukumu

### Hoja za kisheria


Katika shauri hilo, Bashange alijenga hoja kuwa kifungu 44(1) na (2) cha sheria hiyo viko kinyume cha Katiba, vinakiuka misingi ya haki ya asili, vinakiuka haki za msingi na pia vinapingana na dhana ya mgawanyo wa madaraka ya dola.

Bashange, kada na mmoja wa viongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, aliiomba mahakama itamke kuwa vifungu hivyo vinakiuka ibara za 13 (1), (2) (3) (6a) na Ibara za 26 (1) na 29 (1) za Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977.

Hivyo aliiomba mahakama itamke kuwa vifungu hivyo vya sheria LLA ni batili na vifutwe kwenye vitabu vya sheria.

Pia Bashange alisema vifungu hivyo vinakiuka ibara ya 3 (1) na (2), ibara ya 7 (1)(c) na 19 za mkataba wa Afrika wa Haki za watu (ACHPR).

Hakuishia hapo, ameiomba mahakama itoe amri kwa wajibu maombi hao yaani Waziri na AG, kuchukua hatua za makusudi kuhakikisha suala la kuongezwa muda wa kufungua shauri linashughulikiwa na mahakama, ikiwamo pia haki ya kukata rufaa.



Kulingana na vifungu anavyovipinga Bashange, Waziri wa Katiba ya Sheria, baada ya kushauriana na AG anaweza kuongeza muda wa kufungua shauri kwa muda usiozidi nusu ya muda uliotajwa kuhusiana na kesi husika.

Kulingana na kifungu hicho, muda unaoongezwa iwe kabla ya kumalizika au baada ya muda uliowekwa na sheria kumalizika, ni lazima uanze baada ya kumalizika kwa muda uliowekwa na sheria na inataka uanze kuhesabiwa pale amri ilipotolewa.

Bashange amesema kifungu hicho hakina maana na kinajikanganya na kinamnyima mdai haki ya kufungua shauri mahakamani na hivyo kumzuia kufikia milango ya haki katika mahakama na hivyo kufanya kisiwe na maana yoyote.

Mleta maombi aliyewakilishwa na Wakili Daimu Halfan, alieleza kuwa mahakama katika maombi yake kuongeza muda wa kufungua shauri ni mchakato wa kisheria ambao ni sehemu ya kesi inayotaka kufunguliwa na nyongeza ya muda.

Kifungu anachokipinga, kwa mujibu wa Bashange, kinampa mamlaka waziri ambaye ni mhimili wa dola wa Serikali, wakati mamlaka ya kuamua kesi yenyewe ndio yanaachiwa mahakama hivyo, akasisitiza kuwa kifungu hicho kina ubaguzi.

Kwa upande wa wajibu maombi ambao ni Waziri na AG, kupitia kwa Wakili wa Serikali, Narindwa Sekimanga, walipinga shauri hilo wakisema Bashange hakuwa ameonyesha yeye binafsi, ameathiriwa vipi na kutumika kwa vifungu hivyo.

Lakini pia wakasema vifungu hivyo havikiuki Katiba, havina ubaguzi na si kweli kwamba hakina maana. Pia walisema Bashange ameshindwa kuthibitisha madai yake kwa viwango vya kuthibitisha shauri la Kikatiba.

**SUMMONS TO APPEAR (Order V, R (1) of CPC**

**(Substituted service)**

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**ARUSHA SUB- REGISTRY**

**AT ARUSHA**

**CIVIL CASE NO. 40 OF 2023**

**TIB DEVELOPMENT BANK..........................................................1ST PLAINTIFF**

**ATTORNEY GENERAL.....................................................................2ND PLAINTIFF**

**VERSUS**

**MANOTA TRADING COMPANY LIMITED....................................1ST DEFENDANT**

**GAHER INTERTRADE LIMITED................................................:2ND DEFENDANT**

**TO: MANOTA TRADING COMPANY LIMITED & ANOTHER**

**WHEREAS:** The above-named PLAINTIFF has instituted a SUMMARY PLAINT against you, you hereby summoned to appear in this court in person or by an Advocate or Agent duly authorized on 09th day of April, 2024 at 09:30 am before Hon. D. D. Ndumbaro, Judge to answer the claim; and you are directed to produce on that day all the document upon which you intend to rely in support of your defence.

**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of your appearance on that day before mentioned, the plaint will be heard and determined in your absence.

**GIVEN** under my hand and seal of the court this 29th day of February, 2024.

**DEPUTY REGISTRAR**

**ARUSHA**

Daily News, Friday March 15, 2024.